

MWONGOZO WA INSHA F3

1. Hii ni insha ya kumbukumbu.

Ni muhimu mwanafunzi kufuata utaratibu wa uandishi wa insha ya kumbukumbu k.v

- i) Lazima kuwe na anwani ya kumbukumbu
- ii) Majina ya waliohudhuria
- iii) Walituma udhuru
- iv) Ajenda

- a- wasilisho la mwenyekiti.
- b- Kusomwa na kuthibitishwa kwa kumbukumbu za mkutano uliotangulia.
- c- Yatokanayo na kumbukumbu hizo.
- d- Kusajiliwa kwa wanchama wapya.
- e- Ziara ya wanchama.
- f- Usafi wa mazingira.
- g- N.k

(Watahini wahakiki ajenda za watahiniwa zikilenga mada na pia kufikia idadi inayohitajika)

- h- Mambo mengineyo.
- i- Kufungwa kwa mkutano/kufunga mkutano.

- v) Kumbukumbi zenyewe. Kv.
- vi) Kuwe na sehemu ya sahihi ya mwenyekiti pamoja na katibu wake (aliyeandika kumbukumbu hizo)

Mfano

	Sahihi	Tarehe
Katibu.....
Mwenyekiti

2. Insha ya methali.

- Mtuhiniwa anaweza kuanza insha yake kwa kueleza maana ya methali au kuanza moja kwa moja kutoa kisa au visa.
- Sharti mtahiniwa asimulie kis au visa kuthibitisha ukweli wa methali "Fahali wawili wapiganapo ziumiazo ni nyasi"
- Kisa au visa vilenge maana ya methali hii – wazozanapo viongozi/wakuu/wenye uwezo, wanyonge ndio huumia.
- Sharti kisa kilenge pande mbili za methali, jinsi, wenye uwezo walivyo zozana na jinsi wanyonge walivyoahudhiwa na mzozo huo.
- Mtahiniwa anayeshughulikia upande/sehemu moja ya swali au sehemu moja ya methali hajashughulikia swali kikamilifu na akadiriwe vilivyo. Asizoe alama zaidi ya C.

3. Mtahiniwa aanze insha kwa maneno aliyopewa. Kisa chake kihusishe:

- Chanzo cha kuvuja damu.
- Uhusiano wa mwathiriwa na msimulizi.
- Usaidizi aliopewa mwathiriwa.
- Hatima ya tukio hilo.

Tanabahi: Mtahiniwa aliyeanza kisa kwa maneno tofauti, atakuwa amejitungia swali lake.
Kiwango chake ni D- (1 au 2)

- 4.**
- Mwanafunzi anaweza kuzungumzia madhara na faida kisha atoe msimamo wake.
 - Anaweza kuzungumzia madhara pekee pia.

Hoja

Madhara

- Mafuriko hutokea.
- Vifo vya watu na mifugo.
- Nyumba hubomoka.
- Huathiri usafiri – barabarani.
- Mimea huaharibiwa – huoza au hukosa kukua.
- Magonjwa hutokea k.m malaria kwa sababu ya mbu (hakuna masika yasiyo na mbu)

Faida

- Hukuza mimea / miti
- Mandhari huwa ya kupendeza.
- Chakula huwa kwa wingi.
- Maji ya kunywa / kutumia kwa viwanda n.k.
- Samaki na viumbe wa baharini